

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

**Ziara kwa Ubalozi wa Pakistan Jijini Vienna ili Kutaka Kuachiliwa Huru Mara Moja kwa
Mhandisi Naveed Butt!
(Imetafsiriwa)**

Kama sehemu ya kampeni ya kiulimwengu iliyoziinduliwa na Hizb ut Tahrir kutaka kuachiliwa huru kwa Naveed Butt, msemaji wa Hizb ut Tahrir katika Wilaya ya Pakistan, ambaye alitekwa nyara na wakala wa ujasusi wa Pakistan mnamo tarehe 11 Mei 2012 na tangu wakati huo ametoweka na haijulikani alipo, ujumbe wa Hizb ut Tahrir katika Nchi zinazozungumza Kijerumani ulioongozwa na Mhandisi Shaker Assem, mwakilishi kwa vyombo vya habari wa Hizb ut Tahrir katika Nchi zinazozungumza Kijerumani ulitembelea ubalozi wa Pakistan katika jiji la Vienna kufikisha taarifa kutoka kwa Afisi ya Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika suala hili. Mfanyikazi mmoja wa ubalozi huo alipokea taarifa hiyo, akaahidi kuipeleka kwa serikali ya Pakistan na akahakikisha kuwa ubalozi huo utawasiliana na ujumbe huo juu ya suala hilo

Twamuomba Mwenyezi Mungu (swt) aifanye kampeni hii izee matunda yake na aulete uachwaji huru wa haraka wa ndugu yetu Naveed Butt, mbebaji mashuhuri wa Ulinganizi wa Kiislamu.

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Nchi Zinazungumza Kijerumani